FUNZO LA 59

1. Kwa nini Mafarisayo na walimu wa sheria waliwakasirikia wanafunzi wa Yesu?
-Kwa sababu wanafunzi wa Yesu hawakushika mila za wazee.

2. Ni mila gani za wazee?
-Zilikuwa sheria ambazo Mafarisayo walikuwa wametunga ambazo walisema watu lazima wazishike ili wakubalike na Mungu.

3. Je, Mungu anatukubali kulingana na mila tunazoshika?
-La.

4. Je, kufuata mila kutafanya mioyo yetu iwe safi?
-La.

5. Mnafiki ni nini?
-Mnafiki ni mtu ambaye maneno na matendo hayafanani, lakini ni tofauti kabisa.

6. Nabii Isaya alisema nini kuhusu watu hawa?
-Nabii Isaya alisema kuwa watu hawa wanasema kwa midomo yao kwamba wanaamini katika Mungu, lakini kwamba mioyo yao iko mbali na Mungu.

7. Kwa nini Mungu hakukubali ibada ya Mafarisayo?
-Kwa sababu ibada yao ilitoka kwa midomo yao tu, na sio kutoka kwa mioyo yao.



8. Je, Mungu anataka watu waongeze mila zao kwenye Biblia yake?
-La.
-Hatupaswi kamwe kuongeza au kuondoa chochote kutoka kwa kile Mungu alisema katika Biblia.

9. Kwa nini watu hawafanyiwi najisi kwa mikono michafu au na chakula kichafu?
-Kwa sababu mikono michafu na chakula kichafu havigusi moyo.

10. Je, kile tunachokula kinatufanya tukubalike kwa Mungu?
-La.

11. Je, kile tusichokula kinatufanya tukubalike kwa Mungu?
-La.

12. Yesu alisema nini humfanya mtu kuwa najisi?
-Yesu alisema kuwa kile kilicho ndani ndicho kinachomfanya mtu kuwa najisi.

13. Ni maovu gani ambayo yako ndani ya kila moyo wetu?
-Mawazo mabaya, uasherati, wizi, mauaji, uzinzi, tamaa, uovu, udanganyifu, ufisadi, wivu, kashfa, kiburi na upumbavu.

14. Katika mfano ambao Yesu alisema, ni watu gani wawili ambao walikwenda hekaluni kuomba?
-Mmoja alikuwa Mfarisayo na mwingine alikuwa mtoza ushuru.

15. Kwa nini Mungu alimkataa Mfarisayo?
-Kwa sababu yule Mfarisayo hakuamini kuwa alikuwa na moyo mchafu.
-Kwa sababu yule Mfarisayo hakuamini kwamba alikuwa amemkosea Mungu.

16. Kwa nini Mungu alimkubali mtoza ushuru?
-Kwa sababu mtoza ushuru alijua kwamba alikuwa na moyo mchafu.
-Kwa sababu mtoza ushuru alijua kwamba alikuwa amemkosea Mungu.
-Kwa sababu mtoza ushuru alimwomba Mungu amwokoe.

-Siku moja, Yesu aliwauliza wanafunzi wake swali.

Tusome Marko 8:27-28

27-Akatoka Yesu na wanafunzi wake, wakaenda kwenye vijiji vya Kaisaria-Filipi; na njiani akawauliza wanafunzi wake, akasema, "Watu huninena mimi kuwa ni nani?"
28-Wakamjibu, Yohana Mbatizaji; wengine, Eliya; wengine, Mmojawapo wa manabii.

-Lilikuwa swali gani ambalo Yesu aliwauliza wanafunzi wake?

-"Je, watu husema mimi ni nani?"

-Wanafunzi walijibu nini?

-Baadhi ya watu walidhani kwamba Yesu alikuwa Yohana Mbatizaji.



-Baadhi ya watu walidhani kwamba Yesu alikuwa Eliya.

-Watu wengine walidhani kwamba Yesu alikuwa mmoja wa manabii waliofufuka.

-Kwa nini watu walidhani kwamba Yesu alikuwa Yohana Mbatizaji?

-Kwa sababu Mfalme Herode alikuwa amemuua Yohana Mbatizaji, watu wengine walidhani kwamba Yesu alikuwa Yohana Mbatizaji ambaye alikuwa amefufuka.

-Je, Yesu alikuwa Yohana Mbatizaji?

-La.

-Kwa nini watu walidhani kwamba Yesu alikuwa Eliya?

-Eliya alikuwa nani?

-Eliya alikuwa nabii wa Mungu ambaye hakuwa amekufa, lakini alikuwa amechukuliwa mbinguni na Mungu.

-Je, Yesu alikuwa Eliya?

-La.

-Kwa nini watu walidhani kwamba Yesu alikuwa mmoja wa manabii waliofufuka?

-Kwa sababu manabii walikuwa wakisema kila wakati kumhusu Mungu na kuwaita watu watubu.

-Je, Yesu alikuwa mmoja wa manabii waliofufuka?

-La.

-Ni swali gani ambalo Yesu aliwauliza wanafunzi wake?

Tusome Marko 8:29

29-Naye akawauliza, Na ninyi mnasema ya kuwa mimi ni nani? Petro akamjibu, akamwambia, “Wewe ndiye Kristo.”

-Je, Yesu aliwauliza nini wanafunzi wake?

-“Mnasema mimi ni nani?”

-Petro alijibu nini?

-“Wewe ndiye Kristo.”

-Petro alijua kuwa Yesu ndiye Kristo ambaye Mungu aliahidi kwa Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni.

-Petro alijua kuwa Yesu ndiye Kristo ambaye Mungu aliahidi kwa Abrahamu, Isaka na Yakobo.



-Petro alijua kuwa Yesu ndiye Kristo, Mungu Mwokozi.

-Ijapokuwa Yesu alikuwa amewaambia Wayahudi mara nyingi, Wayahudi wengi hawakuamini kwamba Yesu alikuwa Mungu Mwokozi.

-Ijapokuwa Yesu alikuwa amefanya miujiza mingi mbele ya Wayahudi, Wayahudi wengi hawakuamini kwamba Yesu alikuwa Mungu Mwokozi.

-Ikiwa hatuamini kwamba Yesu ni Mungu Mwokozi, tunaweza kuokolewa?

-La.

-Je, Yesu alisema nini baadaye kwa wanafunzi wake?

Tusome Marko 8:30

30-Akawaonya wasimwambie mtu habari zake.

-Kwa nini Yesu aliwaambia wanafunzi wasimwambie mtu yeyote kumhusu?

-Yesu hakutaka watu waamini kwa sababu ya mtu mwingine.

-Yesu alitaka watu waamini kutoka kwa mioyo yao.

-Kama tunamwamini Yesu, basi imani hii lazima itokane na mioyo yetu wenyewe.

-Hatuwezi kumwamini Yesu kutoka kwa mtu mwingine.

-Baada ya hii, Yesu ndipo akaanza kuwafundisha wanafunzi kuhusu yale yatakayofanyika.

Tusome Marko 8:31

31-Akaanza kuwafundisha kwamba imempasa Mwana wa Adamu kupatikana na mateso mengi, na kukataliwa na wazee, na wakuu wa makuhani, na waandishi, na kuuawa, na baada ya siku tatu kufufuka.

-Je Yesu aliwafundisha nini wanafunzi wake kuhusu yale yatakayofanyika?

-Kwamba viongozi wa watu wangemuua Yesu, lakini kwamba atafufuka kutoka kwa wafu baada ya siku tatu.

-Yesu alijuaje kinachokuja?

-Kwa sababu Yesu ni Mungu na anajua kila kitu.

-Hakuna chochote ambacho Yesu hajui.

-Yesu alijua kuwa viongozi wa watu wangemuua.

-Yesu pia alijua kwamba lazima afe.

-Lakini Yesu pia alijua kwamba atafufuka kutoka kwa wafu baada ya siku tatu.



-Je, unakumbuka Yona alikuwa siku ngapi usiku na mchana katika tumbo la samaki mkubwa?

-Siku tatu na usiku tatu.

-Kama vile Yona alikuwa ndani ya tumbo la samaki mkubwa siku tatu na usiku tatu, Yesu pia angekuwa ndani ya tumbo la dunia siku tatu na usiku tatu.

-Kama vile Mungu alimfufua Yona baada ya siku tatu na usiku tatu, Mungu pia atamfufua Yesu baada ya siku tatu na usiku tatu.

-Baada ya hayo, Yesu alichukua Petro, Yakobo, na Yohana kwenda naye juu ya mlima mrefu.

Tusome Marko 9:2-3

2-Hata baada ya siku sita Yesu akawatwaa Petro, na Yakobo, na Yohana, akawaleta juu ya mlima mrefu faraghani, peke yao; akageuka sura yake mbele yao;
3-mavazi yake yakimeta-meta, meupe mno, jinsi asivyoweza dobi duniani kuyafanya meupe.

-Je, ni nini kilichomfanyikia Yesu mlimani?

-Yesu alibadilika sura mbele ya Petro, Yakobo, na Yohana.

-Inamaanisha nini kwamba Yesu aligeuka sura?

-Inamaanisha kwamba Mungu ambaye alikuwa ndani ya Yesu aliangaza nje.

-Ijapokuwa Yesu alikuwa na mwili wa kibinadamu nje, alikuwa Mungu kwa ndani.

-Je, unakumbuka hema ambalo Musa na Waisraeli walijenga jangwani?

-Katika nje ya hema kulikuwa na ngozi za wanyama, lakini ndani kulikuwa na utukufu wa Mungu.

-Watu walipomtazama Yesu, walimwona tu mtu kwa nje.

-Lakini kwa ndani, Yesu alikuwa Mungu.

-Yesu alikuwa Mungu kamili na mwanadamu kamili.

-Ghafla, walionekana wanaume wawili karibu na Yesu.

Tusome Marko 9:4

4-Wakatokewa na Eliya pamoja na Musa, nao walikuwa wakizungumza na Yesu.

-Je, Eliya alikuwa nani?

-Eliya alikuwa nabii wa Mungu ambaye alikuwa ameishi duniani kabla ya Yesu kuzaliwa.



-Miaka mingi iliyopita, kabla ya Eliya kufa, Mungu alikuwa amemchukua kwenda mbinguni.

-Je, Musa alikuwa nani?

-Musa ndiye aliyewaongoza Waisraeli kutoka Misri.

-Miaka mingi iliyopita, Musa alikuwa amekufa, na Mungu alikuwa amemchukua Musa kwenda mbinguni.

-Kwa sababu Eliya na Musa walimwamini Mungu, walikuwa wameishi mbinguni na Mungu kwa miaka mingi.

-Ni vipi Eliya na Musa walirudi duniani?

-Mungu Baba alimtuma Eliya na Musa chini kutoka mbinguni kuzungumza na Yesu.

-Kwa nini Mungu alitaka Eliya na Musa wazungumze na Yesu?

-Mungu alitaka Eliya na Musa wamtie moyo Yesu kwa sababu ya kifo cha Yesu kinachokuja.

-Ni nini kilitokea baadaye?

Tusome Marko 9:5-8

5-Petro akajibu, akamwambia Yesu, Rabi, ni vizuri sisi kuwapo hapa; na tufanye vibanda vitatu, kimoja chako wewe, kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya.

6-Maana, hakujua la kunena, kwa kuwa waliingiwa na hofu nyingi.

7-Kisha likatokea wingu, likawatia uvuli; sauti ikatoka katika lile wingu, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, msikieni yeye.

8-Mara hiyo walipotazama huku na huku, hawakuona mtu pamoja nao ila Yesu peke yake.

-Je, sauti iliyotoka kwenye wingu ilikuwa ya nani?

-Mungu Baba.

-Ni nini Mungu Baba aliwaambia wanafunzi?

-"Huyu ni Mwanangu, ninayempenda. Msikilizeni!"

-Mungu Baba alimaanisha nini?

-Mungu Baba alimaanisha kwamba kweli Yesu alikuwa Mungu Mwokozi, ambaye alimpenda sana.

-Kwa sababu Yesu alikuwa Mungu Mwokozi, Mungu alitaka wanafunzi wamsikilize Yesu.

-Leo, je, Mungu anasema nasi kutoka mbinguni?

-La.



-Kwa nini?

-Kwa sababu yote ambayo Mungu anataka kusema kwetu yameandikwa katika Kitabu chake, Biblia.

-Mungu anataka tumsikilize Yesu na Maneno yake ambayo yameandikwa katika Kitabu cha Mungu, Biblia.